

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KARATU (KARATU WSSA)

Mnamo tarehe 28 Aprili 2022 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu (Karatu WSSA). Majedwali Na 1 hadi 3 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Karatu WSSA.

Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa	
	2021/22	2022/23	2023/24
Majumbani	1,750	2,075	2,128
Taasisi	1,750	2,075	2,128
Biashara	2,000	2,371	2,432
Viwanda	2,000	2,371	2,432
Magati	1,500	1,778	1,824

Jedwali Na. 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa	
	2021/22	2022/23	2023/24
Majumbani	15,000	15,000	15,000
Taasisi	15,000	15,000	15,000
Biashara	15,000	15,000	15,000
Viwanda	15,000	15,000	15,000

Jedwali Na. 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuunganishiwa Huduma (Shilingi/Maunganisho Mapya)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada inayopendekezwa	
	2021/22	2022/23	2023/24

Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019
Taasisi		
Biashara		
Viwanda		

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maji Karatu, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kutekeleza mikakati iliyoainishwa kwenye mpango wa biashara kwa kipindi cha 2022/23-2023/24 na hivyo kuhakikisha uendelevu wa huduma ya maji katika mji wa Karatu. Bei zinazopendekezwa zinapelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa maji, upanuzi wa mtandao wa huduma, kuongeza wafanyakazi na kuongeza uwezo wa kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi**, tarehe **23 Juni 2022**, katika **Ukumbi wa KDA**, Karatu Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maadnishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 30 Juni 2022. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Karatu WSSA yanaweza kupatikana kwenye ofisi za **Makao Makuu ya EWURA** zinazopatikana katika **Jengo la EWURA, Medeli Magharibi, Dodoma** au **Ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini** zilizopo **Ghorofa ya Pili, Jengo la PSSSF, Jirani na Kibo Palace Hotel, Arusha** au kwenye **Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu** zilizopo **Karatu Mjini**.

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
09 Juni 2022